**FOMU NO. S3241**

# SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA JOSIAH

**P.O.BOX 1605 – BUKOBA,**
**Registration No: 4273**
**Phone: +255 753 739 321**

**KAGERA – TANZANIA,**
**Email:Josiahgirlshighschool@yahoo.com.**

**MY DREAM MY DESTINY – NDOTO YANGU UPEO WANGU.**

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA JOSIAH KWA MASOMO YA KIDATO CHA TANO KWA MWAKA WA MASOMO 2025 -2026**

**JINA**________________________________________ **ADMISSION NUMBER** _______________

1. **UTANGULIZI**

   Kwa niaba ya uongozi wa shule ya sekondari ya wasichana Josiah nakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule yetu kwa kidato cha tano. Unatakiwa kuripoti shuleni mapema tarehe **16/06/2025** kwa ajili ya kuanza masomo.

   Shule ya sekondari ya wasichana Josiah yaani **JOSIAH GIRLS' SECONDARY SCHOOL** ni shule ya bweni tu iliyosajiliwa na Wizara ya Elimu kwa namba **S4273.**

   Ni shule inayofuata mtaala wa Tanzania na inafanya mitihani yote ya Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) kwa namba **S3241**. Shule haifungamani kabisa na upande wowote wa siasa wala dini yoyote. Hivyo tunasajili wanafunzi wa kutoka kila eneo la Tanzania na nje ya nchi.

2. **MAHALI SHULE ILIPO**

   Shule ya sekondari ya wasichana Josiah imejengwa katika kijiji cha Ijuganyondo – Manispaa ya Bukoba, Mkoani Kaagera, kilomita sita kutoka katikati ya mji wa Bukoba.

3. **USAJILI**

   Mwanafunzi atasajiliwa shuleni baada ya kufanya mtihani wa usaili. Wastani wa Shule ni alama sitini na tano (65%) kwa kidato cha Tano na sita.

**MICHEPUO INAYOFUNDISHWA HAPA KWA KIDATO CHA TANO NA SITA.**

| MCHEPUO | MASOMO |
|---|---|
| PCM | PHYSICS, CHEMISTRY, ADV. MATHEMATICS, ACADEMIC COMMUNICATION |
| PCB | PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY, BAM, ACADEMIC COMMUNICATION |
| PMC | PHYSICS, ADV. MATHEMATICS , COMPUTER SCIENCE, ACADEMIC COMMUNICATION |
| PGM | PHYSICS,GEOGRAPHY, ADV. MATHEMATICS, ACADEMIC COMMUNICATION |
| CBG | CHEMISTRY, BIOLOGY, GEOGRAPHY, BAM, ACADEMIC COMMUNICATION |
| EBuAc (ECA) | ECONOMICS,BUSINESS STUDIES, ACCOUNTANCY, BAM, ACADEMIC COMMUNICATION |
| H.G.E | HISTORY, GEOGRAPHY, ECONOMICS, BAM, ACADEMIC COMMUNICATION |
| HGL | HISTORY, GEOGRAPHY, ENGLISH, ACADEMIC COMMUNICATION |
| HKL | HISTORY, KISWAHILI, ENGLISH LANGUAGE, ACADEMIC COMMUNICATION |
| HKLi | HISTORY, KISWAHILI,LITERATURE, ACADEMIC COMMUNICATION |
| HGK | HISTORY, GEOGRAPHY, KISWAHILI, ACADEMIC COMMUNICATION |
| EGM | ECONOMICS, GEOGRAPHY, ADV. MATHEMATICS, ACADEMIC COMMUNICATION |

4. **ADA**

**(a). ADA YA MWAKA – KIDATO CHA V-VI.**

Ada ya mwaka ni **Tsh. 2,600,000/=** na inaweza kulipwa kwa awamu nne, kwa **Tsh. 650,000/=** kila awamu

**(b) MICHANGO MINGINE**

| S/No | JINA | KIASI (TSH) | |
|---|---|---|---|
| 1 | "Commitment fee" | | Mara moja |
| 2 | Usajili. | 100,000/= | Mara moja |
| 3 | Kitambulisho. | 10,000/= | Mara moja |
| 4 | Vifaa vya usafi. | 10,000/= | Mihula miwili |
| 5 | Usafiri kwenda hospitali. | 10,000/= | Kila muhula |
| 6 | Sare ya Shule. | 250,000/= | Sketi 2, Shati 2, Koti 1 na T-shirt 1 |
| 7 | Vifaa vya maabara kwa wanaosoma sayansi | 100,000/= | Kila muhula |
| 7 | Ziara ya kimasomo. | 40,000/= | |
| 8 | Sahani, Kikombe na kijiko. | 25,000/= | |
| 9 | Fedha ya kunyoa (kwa wasiosuka) | 4,000/= | Kila muhula |

**MALIPO YOTE YA ADA YAFANYIKE BENKI YA CRDB**akaunti namba **0150215933100** kwa jina la **JOSIAH GIRLS' HIGH SCHOOL NA MICHANGOMINGINE KATIKA**

**BENKI YA NMB ACCOUNT NO. 31810017945.** Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi na kidato anachosoma kisha hiyo ***"pay slip"***iletwe hapa shuleni siku ya kuripoti.

Hakuna malipo yoyote ya mkononi (cash) yatakayopokelewa hapa shuleni au kulipwa kwa simu pia hairuhusiwi. Ofisi haitayatambua malipo ya aina hiyo.

**MAHITAJI YANAYONUNULIWA NA MZAZI**

Kila mwanafunzi aje na mahitaji yafuatayo siku ya kuripoti shuleni aweke alama vitu vyake.

| S/No. | VIFAA | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | REAM YA KARATASI (A4) | 01 |
| 2. | MAFAILI MAWILI (BOX FILE MOJA NA SPRING FILE RANGI YA BLUU AU NJANO MOJA) | |
| 3. | COUNTER BOOKS (QUIRE 3 au 04) | 10 |
| 4. | KALAMU ZA WINO (BLUU au NYEUSI) | ZA KUTOSHA |
| 5. | PENSELI NA VIFUTIO | 03 |
| 6. | PRINCPLES OF PHYSICS XI-XII (SCIENCE STUDENTS) | 01 |
| 7. | A-LEVEL PHYSICS BY ROGER MONCASTER (Physics students) | 01 |
| 8. | CHAND XI AND XII CHEMISTRY (SCIENCE SUBJECT) | 01 |
| 9. | CHAND XI AND XII BIOLOGY | 01 |
| 10. | BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL F. V & F. VI. | 01 |
| 11. | PHYSICAL GEOGRAPHY ZISIT KAMILI 2006<br>PRACTICAL GEOGRAPHY BY ZISIT KAMILI 2016 | 01<br>01 |
| 12. | ADVANCED DICTIONARY (OXFORD) KWA HKL, HGK NA HGL | 01 |
| 13. | TRUCK SUTI YA KIJIVU (ADDIDAS) | 01 |
| 14. | VIATU VYEUSI VYA DARASANI VISIVYO NA KISIGINO KIREFU, | JOZI 02 |
| 15. | VIATU VYA WAZI VYENYE MKANDA NYUMA – RANGI NYEUSI KWA AJILI YA KUSHINDIA | |
| 16. | RABA NYEUPE ZA MICHEZO | JOZI 01 |

| | | |
|---|---|---|
| 17. | SOCKS NDEFU NYEUPE ZISIZO NA UREMBO | JOZI 03 |
| 18. | GODORO FUTI 3 X 6 | 01 |
| 19. | BLANKETI | 01 |
| 20. | SHUKA ZA RANGI YA BLUU | 04 |
| 21. | NDOO YA UJAZO WA LITA 10 | 01 |
| 22. | TAA NDOGO YA SOLAR (DELIGHT) | 01 |
| 23. | SKETI NYEUSI ZENYE MALINDA kwa ajili ya kushindia baada ya darasani. | 02 |
| 24. | T-SHIRT 01 YA KIJANI NA T-SHIRT 01 NYEKUNDU kwa ajili ya darasani. | (NZITO, ZISIZO NA KOLA) |
| 25. | CHANDARUA RANGI NYEUPE 3 X 6 | 01 |
| 26. | MATHEMATICAL TABLE (4 FIGURE) ZA OXFRORD wa sayansi tu. | 01 |
| 27. | TAULO | 01 |
| 28. | BAG NDOGO YA KUBEBEA DAFTARI | 01 |
| 29. | NGUO ZA NDANI, NDALA ZA KUOGEA, DAWA YA VIATU, BRUSH, DAWA YA MENO, MISWAKI, SABUNI ZA KUFULIA, SABUNI ZA KUOGEA (PROTEX/DETOL/DURU) MAFUTA YA KUJIPAKA (YASIYO VIPODOZI), VITAMBAA VYA MKONONI, PEDI NA KITENGE PAIR 01, SOAP DISH 01. | VYA KUTOSHA |
| 30. | SCIENTIFIC CALCULATOR (Isipokuwa wanafunzi wa HKL) | 01 |

5. **MAWASILIANO**

   Mawasiliano yote yafanyike kupitia namba za shule inayoonekana katika fomu hii ambayo ni: **+255 753 739 321/ +255614569321**

6. Wazazi/walezi wote mnaombwa kufuata kalenda ya Shule, tarehe za kufunga na kufungua shule.
7. Kila mwanafunzi atapaswa kuvaa sare rasmi ya shule wakati wote awapo shuleni na nje ya shule lakini siyo kipindi cha likizo.
8. Pamoja na fomu hii tunaambatanisha na SHERIA za Shule. Mwanafunzi azisome vizuri na kuzielewa ipasavyo.

# SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA JOSIAH

**P.O.BOX 1605 – BUKOBA,**
**Registration No: 4273**
**Phone: +255 753 739 321**

**KAGERA – TANZANIA,**
**Email:Josiahgirlshighschool@yahoo.com.**

**MY DREAM MY DESTINY – NDOTO YANGU UPEO WANGU.**

---

MAELEZO MUHIMU YA MWANAFUNZI (Fomu hii ijazwe vizuri kwa herufi kubwa na iletwe shuleni siku ya kuripori)

Majinaya mwanafunzi (Majina matatu)_____________________________________________

Shule anayotoka (ya msingi au sekondari kama anahamia) ______________________________

Mahali ilipo: MKOA:________________ WILAYA:___________________

JINA LA BABA/MLEZI___________________________________________ SAINI:__________

KAZI:___________________________________________

SIMU:_______________________________________

JINA LA MAMA/MLEZI_________________________________________ SAINI:___________

ANAPOISHI: MKOA:______________________________ WILAYA:_______________________

KAZI:_________________________ SIMU:___________________________________

**WAGENI WA MWANAFUNZI**

1. PICHA YA MZAZI/MLEZI

2. PICHA YA MZAZI/MLEZI

JINA:_______________________

UHUSIANO:________________

SIMU__________________

JINA:_________________

UHUSIANO:___________

SIMU:_________________

# SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA JOSIAH

**P.O.BOX 1605 – BUKOBA,**
**Registration No: 4273**
**KAGERA – TANZANIA,**
**Phone: +255 753 739 321**
**Email:Josiahgirlshighschool@yahoo.com.**

**MY DREAM MY DESTINY – NDOTO YANGU UPEO WANGU.**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

1. STUDENTS' NAME_________________________________________________ DATE_______________
2. AGE:__________________ HEIGH (CM)_____________ WEIGHT (KG)________
3. BLOOD EXAMINATION (HAAEMOGLOBIN)_________________________
4. BLOOD GROUP:________________
5. ANY ABNOMALITIES NOTE:
   (i).________________________________________________________________________________
   (ii).________________________________________________________________________________
6. TB________________________________________________________________________________
7. STOOL_____________________________________________________________________________
8. URINE ANALYSIS_____________________________________________________________________
9. EYES______________________________________________________________________________
10. EARS______________________________________________________________________________
11. CHEST_____________________________________________________________________________
12. ANY CHRONICAL COMPLICATION e.g.
    (a) ASTHMA________________________________________________________________________
    (b) ABNORMAL HEADACHE______________________________________________________________
    (c) INABILITY TO EAT CERTAIN FOOD____________________________________________________
    (d) SKIN DISEASES___________________________________________________________________
13. ANYTHING ELSE THAT SCHOOL HEALTH STAFF SHOULD KNOW___________________________________________________________________
14. ANY TREATMENT GIVEN OR RECOMMENDED______________________________________________________________

______________________________________________________________________

SIGNATURE OF EXAMINER AND OFFICIAL STAMP_______________

**JOSIAH GIRLS' SECONDARY SCHOOL**
**P.O. BOX 1605, BUKOBA.**
**Simu: +255 753 739 321**

## SHERIA, MAELEKEZO NA WAJIBU WA MWANAFUNZI

Zifuatazo ni baadhi ya sheria ambazo kila mwanafuzi wa Josiah Girls Secondary school anapaswa kuzifuata. Zipo sheria zisizoandikwa ambazo mwanafunzi anatakiwa akili ya kuzaliwa (common sense) ili aishi vizuri katika jamii ya shule na nje ya shule.

1. **HESHIMA**

(a). Lugha chafu ya mitaani hairuhusiwi shuleni, aidha lugha ya kiingereza ni lazima kuzungumzwashuleni.

(b). Mwanafunzi anatakiwa kuwasalimia walimu na wanafunzi wenzake shuleni na watu wengine wanaomzidi umri popote anapokutana nao.

(c). Mwanafunzi aheshimu, athamini na ashiriki kazi za iana zote shuleni. Pia anatakiwa kushiriki kazi za nje ya darasa jinsi atakavyoelezwa na uongozi wa shule.

(d). Yafuatayo hayaruhusiwi shuleni

- Kuvuta sigara, Kunywa pombe, madawa ya kulevya n.k
- Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu zisizotunzwa, mapambo n.k
- Ugomvi.
- Kuvaa nguo zisizo za heshima mfano vipedo, vimini n.k

(e). Mwanafunzi aheshimu alama za taifa

- Bendera ya taifa.
- Picha za viongozi wa serikali.
- Nembo ya taifa (coat of arm).
- Wimbo wa taifa, Tanzania Nakupenda, wimbo wa shule na wimbo wa afrika masharíki.
- Fedha za Taifa.

(f). Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kutunza mali ya shule kama majengo, samani, ofisi zote, vifaa, vitabu n.k

(g). Mwanafunzi anatakiwa kujiheshimu yeye mwenyewe, wanafunzi wenzake, viranja na wafanyakazi wote shuleni.

(h). Mwanafunzi hatakiwi kujiingiza kwenye masuala ya vyama vya siasa.

(i). Kelele, na usumbufu wowote ndani na nje ya madarasa haviruhusiwi.

2. **MAHUDHURIO**

(j). Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia utaratibu wa shule katika shughuli za kila siku. Lazima awepo mahali anapotakiwa kulingana na ratiba ya shule.

(k). Maandalio ya jioni (prep.) ni sehemu ya mafunzo, hivyo mwanafunzi anatarajiwa kuhudhuria na kuyapaka umuhimu unaostahili.

(l). Muhula wa masomo unapoanza shuleni ni kwa wote (wanafunzi, walimu na wafanyakazi).Hakuna mwanafunzi atakayevumiliwa kwa tabia ya kuchelewa shule isipokuwa kama kunajambo la dharura na ambalo litathibitishwa na wahusika.

(m). Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vya masomo kama inavyooneshwa katika ratiba ya shule. Ajitume na kuonesha juhudi katika masomo. Atakaye onesha ulegevu, udhaifu na kutojali shughuli za kitaaluma atachukuliwa hatua na baraza la walimu pamoja na bodi ya shule.

**3. MABWENI**

(i). Mabweni ni mahali pa wanafunzi kulala wakati wa usiku tu na si mahali pa kusomea. Hivyo, wakati wa masomo na shughuli nyingine, mabweni sharti yafungwe, taa zizimwe na mabomba ya maji yafungwe. Vivyo hivyo na wakati wa maandalio ya siku hairuhusiwi mwanafunzi kubaki bwenini, pasipo na sababu maalum ila kwa kibali maalum.

(ii). Taa zote za ndani ya vyumba zitazimwa saa 4:30 usiku na wanafunzi kulala bila kelele nausumbufu wowote ule.

**4. SARE YA SHULE**

(i). Sare rasmi ya shule ni ile inayonunuliwa shuleni. Hivyo sharti ivaliwe:

- Darasani
- Mwanafunzi anapotoka nje ya shule kwa sababu yoyote ile.
- Mwanafunzi anaposafiri kuja na kwenda likizo.

(ii). Mwanafunzi atakuwa na mavazi mengine rasmi kwa shughuli za nje kama kazi za mikono namichezo.

(iii). Mwanafunzi anatakiwa kuvaa viatu vya rangi nyeusi tu. Visiwe na visigino, virefu, viwe vyaheshima.

(iv). Mwanafunzi atalazimika kulipa na kupewa kitambulisho cha shule ambacho atakitumia nakukionesha wakati wowote akiwa nje ya shule na hasa safarini.

**5. HAYA HAYARUHUSIWI KULETWA SHULENI.**

Urembo, Radio, camera, simu za mkononi, mishumaa, vibatari na koroboi haviruhusiwi shuleni.Mwanafunzi anayekiuka onyo hili, atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kutengwa na shule.

**6. MIPAKA YA SHULE**

Ieleweke wazi kuwa mwanafunzi anakubaliwa kuandikishwa shuleni kwa minajiri ya kusoma na kujifunza. Vile vile, mihtasari ya masomo na mihula imepangwa ili mwanafunzi apate elimu inayostahili. Kwa misingi hiyo, mwanafunzi hatarajiwi kuondoka shuleni na kukosa mafunzo kwa sababu zisizoeleweka kwa uongozi wa shule.

**Hivyo:**

(a). Mwanafunzi asitoke nje ya shule bila kibali maalum cha maandishi.

(b). Mwanafunzi anayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya shule arejee shuleni kabla ya saa 12:00 jioni.

(c). Kwa mwanafunzi aliyetoka nje ya mipaka ya shule ni marufuku kutembelea vilabu vya pombe, nyumba ya starehe na nyumba za wageni.

(d). Japo sehemu zifuatazo zimo ndani ya mipaka ya shule, mwanafunzi haruhusiwi kuzitembelea ama kuingia bila rukhusa maalumu.

- Chumba cha walimu (staff room).
- Ofisi zote za shule.
- Maabara.
- Jiko.
- Nyumba za wafanyakazi wote (walimu na wasiokuwa walimu).
- Maktaba.

**7. USAFI**

Kila mwanafunzi anatarajiwa kuzingatia usafi wake binafsi na wa mazingira.
Mwanafunzi anatakiwa kushiriki shughuli za usafi wa bweni, darasa, bwalo na mazingira yote ya shule. Mwanafunzi azingatie usafi kama sehemu muhimu ya maisha yake.

**8. BWALO LA CHAKULA**

Hii ni mojawapo ya majengo muhimu shuleni. Ni lazima jengo hili liheshimiwe na kutunzwa. Kila mwanafunzi anapashwa:
(i). Kutunza usafi wa ndani na nje ya jingo.
(ii). Kuwahi wakati wa chakula ili kuruhusu usafi ufanyike na wenye zamu baada ya chakula.
(iii). Kutunza meza, viti na vifaa vingine vya chakula.
(iv). Chakula kinachoruhusiwa shuleni ni kile kinachotayarishwa na kuandaliwa na shule na kuliwa bwaloni tu.

**MUHIMU**: Mwanafunzi haruhusiwi kuingiza chakula shuleni wala kulia chakula bwenini. Ni mwiko mwanafunzi kutayarisha chakula chake au kuwa na tabia ya kula ovyo.

**9. MAKOSA MAZITO**

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule:
- Wizi (aina zote)
- Uasherati na ushoga
- Kulala kwenye kitanda kimoja
- Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya
- Makosa ya jinai
- Kupiga / kupigana
- Kuharibu makusudi mali ya mwingine au ya umma
- Kudharau bendera ya Taifa na alama nyingine za taifa
- Kuolewa
- Kupata mimba
- Kutoa mimba
- Kugoma, kuchochea kuongoza uvunjifu wa amani na usalama wa watu na mali. Kukataa adhabu kwa makusudi.
- Kuficha kwa makusudi taarifa ambayo inaweza kusaidia katika kuzuia kutokea kwa jambo baya na la hatari.
- Kufanya vitendo vinavyoweza kuhatarisha maisha yake na wengine kama vile kutishia kujiua au kuua wengine.
- Kughushi mitihani au wizi wa mitihani kukataa na kutofanya mitihani na mazoezi.
- Kuchelewa kuwasili shuleni baada ya likizo kwa mfululizo bila sababu ya maana.

NB: Hati ya kuridhia sheria na maelekezo haya inatakiwa kujazwa, kusainiwa nakurejeshwa shuleni kabla ya kusajili mwanafunzi

**10. DINI**

(i). Kila mwanafunzi anaruhusiwa kuhudhuria na kuabudu kwenye dini yake ambayo inafahamika kwa wazazi / walezi wake.

(ii). Kamwe mwanafunzi hataruhusiwa kubadili dini anapokuwa shuleni kinyume na matakwa ya wazazi / walezi wake. Mwanafunzi / wanafunzi hao wanazifahamu na kuziridhia.

(iii). Kila mwanafunzi anapaswa kuvumilia tofauti za wengine kidini. Shule haitavumilia wanafunziwenye imani zilizopindukia (religious extremists) ambao wanaweza kusababisha uvunjifu wa amani shuleni na kuleta madhara kwao wenyewe au kwa wengine.

**11. WAGENI**

(i). Wageni wanaoruhusiwa kutembelea mwanafunzi ni wale tu ambao watakuwa wameoneshwa katika fomu ya mwanafunzi aliyoijaza kabla ya kuanza masomo.

(ii). Wageni wa wanafunzi watafika shuleni siku na wakati utakaojulishwa kwao na walimu.

(iii). Siku maalum ya wazazi / walezi wote kufika shuleni kwa madhumuni ya kuona maendeleo ya wanafunzi na shule kwa ujumla itateuliwa na baraza la walimu.

(iv). Mzazi mmoja au kundi dogo la wazazi wanaweza kuitwa shuleni kwa minajiri ya kujadiliana na uongozi wa shule kuhusu maendeleo ya watoto wao.

(v). Mzazi / mlezi kufika shuleni kwa shabaha ya kutaka kujua maendeleo na tabia ya mwanae.

**MUHIMU:** Nje ya utaratibu huu, wazazi wanaombwa kujizuia kufika shuleni. Wazazi wawaachienafasi watumishi wa shule na wanafunzi kazi zao.

**12. TAARIFA**

Mzazi / mlezi wa mwanafunzi atapata taarifa kuhusu tabia mwenendo na maendeleo ya mtoto wake kwa njia ya:-

(i). Ripoti ya mwanafunzi kwa mzazi / mlezi inayotayarishwa na walimu kila mwisho wa muhula. Mzazi / mlezi anashauriwa ahakikishe ripoti hii anaipata. Ikiwa ataikosa (kwa ujanja wa mtotowake) awasiliane na uongozi wa shule. Mzazi / mlezi anapopata taarifa hii, anaombwa kuifanyiakazi kwa kushirikiana na uongozi wa shule.

(ii). Mzazi / mlezi kufika shule kuonana na uongozi wa shule.

(iii). Mawasiliano kati ya mzazi na uongozi wa shule kwa njia ya simu au barua.

(iv). Kuhudhuria siku ya wazazi.

______________

**MKUU WA SHULE**

**MY DREAM MY DESTINY - NDOTO YANGU UPEO WANGU**

**"FAILURE TO USE COMMON SENSE IS THE SAME AS BREAKING SCHOOL RULES."**